NGUVU ya MAOMBI

Semina ya Mafunzo katika Maombi ya Kikundi Nguvu

MTUME PAUL GALLIGAN

NGUVU

ya

MAOMBI

Imeandikwa

na

MTUME PAUL GALLIGAN

YALIOMO

Maombi: utangulizi

Sehemu ya kwanza: kuwa haki na mungu (kujiandaa kwa maombi)

- Kufanywa haki
- Kutakaswa
- Kutukuzwa

Sehemu ya pili: yesu kristo

- Mtazamo wa maombi
- Funguo za kufaulu kwa maombi

Sehemu ya tatu: sifa katika maombi

- Kutazama sifa kupitia maandiko
- Tumeamriwa kusifu
- Sifa katika agano jipya
- Maombi na nyimbo za sifa

Sehemu ya nne: vipawa vya Roho Mtakatifu na maombi.

- Roho Mtakatifu na Yesu
- Roho Mtakatifu na mwamini
- Kuzaliwa kwa kanisa
- Ni nani awezaye kupokea Roho Mtakatifu?
- Ni vipi baadhi ya vipawa vya Roho Mtakatifu?
- Vipawa zafanya kazi namna gani katika mkutano wa maombi?
- Ni nani awezaye kutumia vipawa vya Roho Mtakatifu?
- Vipawa vyaleta utukufu wa Mungu.

Sehemu ya tano: silaha za mungu.

- Utangulizi
- Kuwa na nguvu katika Bwana
- Mshipi wa kweli
- Dirii ya haki
- Viatu vya injili ya amani
- Ngao ya imani
- Upanga wa Roho
- Maombi

Sehemu ya sita: silaha za vita vya kiroho

- Damu ya Mwana kondoo
- Neno la ushuhuda wao (wetu)
- Hawakuyapenda maisha yao mpaka kufa
- Silaha zingine

Sehemu ya saba: Maombezi

- Maombezi - Kitendo cha kwenda katikati
- Yesu kama muombezi
- Kudumu ndani ya Kristo Yesu - Kuomba kwa kukubaliana
- Dhihirisho

MAOMBI: UTANGULIZI

Yohana 15:3 "Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia".
Zaburi 12:6. "Maneno ya Bwana ni maneno safi, ni fedha iliyojaribiwa kalibuni juu ya nchi; Iliyosafishwa mara saba".

MAOMBI NI MAWASILIANO NA MUNGU

Mungu ametupa neno lake, Biblia, ambalo ni neno lake kwetu. Mungu huwasilianan nasi kupitia neno lake. Ni njia yake aliyochagua. Yesu Kristo anataburika kama neno la Mungu katika Yohana sura ya kwanza. Yeye ndiye neno (lililoandikwa) aliyekuwa na Mungu pale mwanzo, aliyekuwa Mungu, na akafanyika mwili na akaishi nasi (***Yohana 1: 1,14).*** Yesu anatuambia neno lake kwetu linatuosha. Tunaposikiza kwa kuyasoma maandiko, Bwana atatuzungumzia. Kuna njia zingine ambazo Mungu hutuzungumzia (kama kupitia ndoto, maono na unabii) lakini neno lake kwetu kupitia biblia ndio njia ya msingi. Mwandishi wa zaburi yuasema neno lake ni safi. Kusikia kutoka kwa Mungu ni ya thamani na ni funguo ambazo zafanya maombi yawe ya kweli, hai na yatende kazi.

KUYAFAHAMU MAOMBI

Mungu hujibu maombi namna gani? Yesu alijibu aje maombi aliyoulizwa na wenye mahitaji? Je ilikuwa tu ni ombi? Je alitumia njia moja tu kujibu? Imani ndio funguo, aliotufunza Yesu, lakini sio imani kipofu. Imani ya kibiblia huja kwa "***kusikia***" neno lake (***Warumi 10:17). "Katika imani yenu tieni na wema na katika wema wenu maarifa … maarifa katika Bwana wetu Yesu Kristo***" (***2Petro 1:5-8).*** Twaweza kujifunza mengi katika kujifundisha maandiko kuhusu maombi na imani hukua wakati hekima ya kweli inakua. Yesu kama mwanadamu alikuwa akiomba sana, na aliwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba, kwa kuwafunza moja kwa moja, kupitia mafumbo na kuwaonyesha. Paulo anatuhimiza kuomba sana na kutuombea katika maneno kadha ya barua zake. Anatufundisha umuhimu wa maombi ya kila muamini, kwa wale wanaohubiri na kufundisha, na katika ulimwengu wa vita na ushindi.

KUSALI KWA MUNGU

Kusali kwa Mungu kuna msingi wakimaandiko, "…***hoja zenu na zijulikane na Mungu***" **(*Wafilipi 4:6).*** Hata hivyo, kuna mengi kuhusu maombi yaliyojibiwa katika kusali kusikokoma. Daudi alimuuliza Mungu mwelekeo fulani: "***Je, niende nikawapige hao Wafilisti?" (1 Samweli 23:2 na maeneo mengine).*** Mungu angalimuambia lakutenda. Maelekezo ya Mungu yalikuwa machache, kama yalikuapo. Wakati kipofu alimjia Yesu kwa uponyaji ***(Yohana 9:6),*** Yesu alitema mate chini kwanza, akayafanya matope na kumpaka machoni, kisha Yesu akamtuma akaoge katika kisima cha Siloamu**.** Kulikuwa na agizo ambalo lilihitaji utiifu wa imani. Huyo kipofu alitii na alirudi akiona (***aya7)***

JAWABU ZA MUNGU NI ZA KIPEKEE.

Maandiko yake yako wazi: watu wa Mungu wapaswa kuomba bila kukoma (1 ***Wathesolonike 5:17***); lakini pia twapaswa kukua katika ufahamu wa mapenzi ya Bwana. Napendekeza twapaswa kushawishika kusali na kuuliza Mungu maarifa maalum ya vile angependa jawabu liwe. Katika ***Waefeso 1:17*** Paulo anaomba, "***Mungu wa Baba wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye".*** Paulo anaendelea kuombea mambo matatu tupasayo kujua kwa (ufunuo): "***macho ya mioyo yenu yetiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi ulivyo, na utajari wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo, kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake***" (***aya 18-19a).***

Kwahitajika kuwa na mafunzo juu ya maombi ili watu waelewe ya kwamba miujiza ya Mungu ni ya kipekee, haitendeki kwa wingi. Mara kwa mara ni ya kibinafsi, na tofauti kwa kila mtu, wakati mwingine zikihitaji toba ama kitendo cha utiifu, ingine yabadilika kwa watu binafsi kwa sehemu ama kulingana na vile anamchukua Mungu. Mungu sio tarakilishi; yeye Mungu yu hai na anatenda, Mungu wa kibinafsi, anayefahamu hali ya mwanadamu kikamilifu**.**

> ***Yohana 15:7 "Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa".***
> ***Aya 8*** Maombi yaliyojibiwa yanamtukuza Mungu Baba, na ni njia ya mazao yetu, na dhihirisho ya uanafunzi wetu.

Hebu natusonge mbele kumjua Bwana na kuhisi mkono wake wa nguvu wa uponyaji!

MUNGU ANALIITA KANISA LAKE KWA MAOMBI

Kuna wito wa maombi kutoka kwa Mungu wakati huu**.** Watu kanisani katika taifa letu wanasikia wito huu. Kutoka 1994, na mapema katika sehemu fulani katika kanisa la ulimwengu, Mungu ameachilia kipawa cha maombezi kama njia mpya kwa visa fulani kwa njia ya kushangaza sana. Watu wamehisi uchungu mkuu ndani ya roho, pamoja na kuugua na ishara zinazoonekana. Kumekuwa na kuachiliwa kwa kuzalisha kwa kiroho ***(Warumi 8:22-27).***

Katika mwaka wa 1994, nilihusika katika kuandaa washa za maombi. Hii imejulikana kwa maana Mungu amekusanya waombezi na wale wanaotamani maombi. Mungu amekua akisaidia wote kusikia sauti yake vizuri. Wakati mwingine watu wamehusika kuomba mara ya kwanza katika vikundi. Kuna wengine kwa mara ya kwanza wamepokea jawabu kutoka kwa Mungu. Kwa wengi wetu maombi ya vikundi yamekuwa furaha kwetu. Maombi ya ushirika yamekua ya zamu (maombi ya kupokeana). Vikundi kama hivyo vimeleta himizo na ushirika wa maombi ya kushiriki.

Wito huu wa maombi unaonyesha vile Bwana anatenda na wa kristo wengi duniani na inaongezeka mwaka baada ya mwaka. Juzi mzee kutoka thehebu moja la kanisa alishiriki vile Mungu ameinua waombezi kanisani mwao mnamo mwaka wa 1996. Mke wa mchungaji kule Yangon, Myanmar (Rangoon, Burma), alishiriki katika mapema 1997 yakwamba yeye ni sehemu ya mwondoko wa AD2000 wa maombi katika nchi yake. Mwanzo wa 1997, nilisikia mwito wa Mungu wa maombi kwa kanisa lake katika taifa letu la Australia tumaanishe kimaombi. Ninaamini kanisa likiitikia kwa wito na kutumia muda kumngojea katika maombi, kibinafsi na katika vikundi, yeye ataonyesha mapenzi yake na aanze kutembea katika taifa. Australia ingali

haijaona ufifio unaotanda ambao utasababisha uzima wa taifa**.** Wengi waamini ufifio kama huo unakuja.

JAWABU ZAKE

Tumeona jawabu nyingi sana kwa maombi kanisani mwetu, katika mji wetu, hali zetu na taifa. Tumeona mkono wa Mungu katika mabadiriko ya kisiasa; tumeshuhudia mvua ikija kuzima moto wa vichaka, na wakati wakupendeza, wa jua ukifuata; tuna mikutano ya wachungaji ya kila juma ya maombi na ushirika katika jiji letu ***(***umoja ni uhakika unaokua na wa kuhimiza); Tumefurahia wakati wa ajabu wa kutebelewa na Roho Mtakatifu wa Mungu kanisani mwetu kwa zaidi ya miaka. Haya ni machache tu.

KUWA HAKI/SAWA NA MUNGU

Ni muhimu kwetu kukusanyika na kumtafuta Bwana. Katika sehemu hii, tutatumia mda tumkaribie Mungu hatua kwa hatua**.** Tutafuata mfano uliotumika katika hema ya Musa.
Sehemu ya kwanza ni kuja kwenye madhabahu ya kuteketeza ambapo dhabihu zilitolewa kufunika na kuchukua dhambi. Madhabahu yalilenga msalaba. Wakati makuhani walikuja kwa hema ya Musa waingie na wafanye huduma yao ya kikuhani mbele ya Bwana, hatua ya kwanza ilikuwa waje kwa madhabahu ya shaba na kutoa dhabihu iliyohitajika kufunika dhambi zao. Basi twaja msalabani na kuzikiri dhambi zetu kwa Mungu, tukiomba msamaha kupitia Yesu. Yeye alijitoa kwetu.

KUHESABIWA HAKI

Tunahesabiwa haki

Warumi 4:25 "*Yesu Bwana wetu alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili tuhesabiwe haki".*
Yesu Kristo anatufanya haki kupitia kufa na kufufuka kwake. *"Tunahesabiwa haki kwa damu yake"* ***(Warumi 5:9).***

Warumi 5:1 *"Tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, Kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo".*

Warumi 10:9 *"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka".*

Unaamini nini ndani ya moyo wako leo? *"Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa*" (**2 *Wakorintho* 13:5**). Tunakiri kile tunaamini ndani ya mioyo yetu kuhusu Yesu Kristo.

Waebrania 3:1 *"Mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu Yesu".* Yeye ni kuhani wa rehema na mwaminifu aliyefanya suluhu kwa dhambi zetu, aliyeteswa, alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wanaojaribiwa ***(Waebrania 2:17-18).*** Ni kupitia Yesu Kristo pekee ambapo twaweza kufanywa haki na Mungu. Yeye anatutakasa na kutufanya tukubariwe na Mungu ***(Warumi 12:1).***

Kukiri kwa dhambi

1 Yohana 1:8-9 "*Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo ndani mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote".*
1 Yohana 1:7 *"Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote*".

Twaweza na twapaswa kuja mbele ya Bwana kumuuliza atakaze mioyo yetu. Wakati mwingine yapasa tuzikiri dhambi zetu mmoja na mwingine ***(Yakobo 5:16)*** kabla ya uponyaji uje.

Kupokea na kupeana msamaha

Yesu alisisitiza katika mafundisho yake ya kwamba msamaha wa Mungu una masharti juu ya msamaha wa dhambi kwetu na wengine. Twayaomba haya katika sala ya Bwana; Yesu akayahimiza haya tena mara tu baada ya kupatiana ombi katika ***Mathayo 6:14-15*.** Tafathari funua hapo sasa.

Ujiulize - Ninahitaji kusamehe mtu – pengine thehebu lililoniumiza - pengine ni idara kama shule au idara ya serikali? Kama Roho Mtakatifu akikuonyesha mtu au idara ambayo haujasamehe, uliza Mungu akupe neema yake ili uweze kusamehe. ***Warumi 5:6*** yatuambia Kristo alikufa kwa wasiomjua Mungu na ***(aya 8)*** yatuambia alitufia tukiwa tungali wenye dhambi. Neema ya msamaha inapatikana kupitia msalaba. Ni kitendo cha kujitakia kitokanacho na moyo wa imani ndani ya Yesu Kristo, kwamba tusameheane, lakini ni neema ya Bwana inayowezesha haya yafanyike.

Wakati mwingine kuwasamehe wale wametuumiza sana kwa ndani *(*maumivu ya aina yote, thuluma, matisho*)* yaonekana kama haiwezekani. Twahitaji msaada wa Bwana. Wakati Yesu alipokuwa akifa msalabani, baada ya kuteseka vibaya mikononi mwa wasiomjua Mungu, alimuomba Babaye kuwasamehe ***(Luka 23:34).*** Kama kusamehe ni vingumu sana kwako, lakini utataka kusameheana ili usamehewe na usetwe huru, uliza Yesu amsamehe mtu huyo: "***Baba msamehe …., na umlete kwa toba kwa jina la Yesu"***

UTAKASO

Tunatakaswa

Hatua ya pili ya kuhani ilikuwa aoge kwenye birika ya shaba. Hii inaweza tafsiriwa kama kuoshwa kwa maji ndani ya neno lake ***(Waefeso 5:26 na Yohana 15:3)*** na hivyo ndivyo tunavyofanya tunapokiri neno la mungu, tukiliamini ndani ya mioyo yetu.

Neno la Mungu linatutakasa ***(Yohana 17:17).*** Hivi ni tunawekwa wakfu kwa Mungu na kwa kusudi lake kwa maisha yetu. Neno la Bwana latawala tabia zetu.

Tunawekwa wakfu kwa Mungu kwa njia ya imani ndani ya Yesu kristo ***(Matendo 26:18, 1Wakoritho 1:2)*** na kazi ya utakazo ya Roho Mtakatifu ndani ya maisha yetu **(*Warumi 15:16).***

Twaitoa miili yetu kuwa dhabihu iliyo hai kwa Mungu ***(Warumi 12:1).*** Dhabihu kama hiyo ni *"takatifu* na ya *kupendeza"* ibada yenu "*yenye maana*".

Mavazi ya Kikuhani

Baada ya kuhani kuoga kwenye birika ya shaba aliyavaa mavazi ya kitani ya kikuhani**.**
Vazi la kitani linazungumzia haki; tunafanywa haki kwa imani katika kifo chake cha ushindi cha Yesu Kristo msalabani. Twapaswa "*kumvaa Bwana wetu Yesu Kristo **(Warumi 13:14)** wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake*".

Kuhani sasa ametakaswa, amewekwa kwa kumtumikia Mungu katika pahali patakatifu. Alivikwa mavazi ya kikuhani. Mavazi haya yalikuwa matakatifu na kuhani naye ametakaswa kupitia damu ya dhabihu **(*Waebrania 13:12)*** na kuoshwa **(*Yohana 15:3).***

Kuhani alifanya huduma gani baada ya kufanywa haki na kutakaswa? Alipaingia pahali patakatifu kutengeneza/kukata utambi wa kinara, akiangalia kama kuna mafuta ya kutosha kuwezesha nuru iangaze. Aliweka mikate juu ya meza ya mkate wa Bwana kila siku. Aliupuliza uvumba katika madhabahu ya uvumba, mbele ya saduku la Agano, ambayo ilikuwa mbele ya kitambaa ndani ya patakatifu pa watakatifu**.**

Twapokea aje vazi hili la kikuhani?
Twastahili ***"kuvikwa uwezo utokao juu" (Luka 24:49b).*** Twahitaji kipawa na uwezo wa Roho Mtakatifu ndani ya mioyo yetu ili tutakaswe kikamilifu, kuvikwa na kuwezeshwa kuingia katika uwepo wake.

KUTUKUZWA

Warumi 8:29-30 *"Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza"*. Mungu anakusudia kuwatakaza waamini kikamilifu (***1Wathesalinika 5:23)*** ili awatukuze, hivyo ni, aufunue utukufu wake kupitia hao (***Yohana 17:22).*** Hili ndilo kusudi la Mungu lililo wazi. Hawezi kufunua utukufu wake kwa wenye dhambi lakini kupitia watakatifu, waliotakaswa.

Ni makusudi ya Mungu kufunika watu wake na utukufu wake (***Isaya 4:2-6***). Katika bustani ya Edeni, Adamu na Eva walikuwa *"uchi na hawakuona haya*" (***Mwanzo 2:25),*** lakini baadaye waliogopa kwa sababu walikuwa "*uchi*" (***Mwanzo 3:7-11***). Ni nini kilibadilika? Dhambi ilikuwa imeingia kupitia kutotii kwao kwa maagizo wazi ya neno la Mungu. Walipoteza kifuniko cha Mungu cha utukufu; hawangeweza tena kutembea na uso wazi mbele ya Bwana; walikuwa sio watakatifu, wakihitaji kufanywa haki na kutakaswa. Kisha Mungu angewafunika tena kwa utukufu wake. Kwa hakika haya hayakuwezekana, na hayangewezekana, kutenda mpaka Yesu aje na amwage damu yake kwa kuwa haki na kutakaswa kwetu. ***Wagalatia 3:27*** yasema "*maana ninyi nyote mlibatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo*". *Warumi 13:14* "*Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuasha tamaa zake*". Kuna kifuniko cha waamini ndani ya Kristo. Ni kifuniko cha utukufu ***(Isaya 4:5).***

2 Wakorintho 3:18 *"Lakini sisi zote, kwa uso usiotiwa utaji, tukirudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho*". Aya hii ni utimilifu wa agano jipya wa huduma ya kikuhani katika madhabahu ya uvumba. Madhabahu ya uvumba yalikuwa nje ya kitambaa na utukufu ulikuwa ndani ya kitambaa katika patakatifu pa watakatifu. Sasa twaweza kumkaribia Mungu kwa uso uliowazi ***(uliofunuliwa, bila kitu kilichofichwa, hakuna aibu ama hukumu ndani).*** Tunapoomba na kuabudu katika Roho na kweli, tunabadilishwa, tunaguzwa na utukufu wake na kubadilishwa katika mfano wake. Halleluyah!

ZOEZI LA SEHEMU YA KWANZA

Wakati mwingine kuna mambo yaliyo ndani yetu ambayo ni ya giza. Tunaweza kumkaribisha Yesu aje katika kila chumba cha maisha yetu. Huu unaitwa uponyaji wa ndani. Mungu anatamani tuje kwa nuru ya upendo wake na neema kikamilifu, tukipokea uponyaji kutokana na majeraha ya kale na upungufu, tukija katika utimilifu ndani ya Kristo.

Zoezi hili litamsaidia muhusika kuhisi njia ya maombi ya kikundi ikiongoza kwa toba na msamaha – pia kama nafasi ya kupokea uponyanji wa Mungu wa ndani, na pia kutumia muda wao kwa watu wengine**.**

a) Katika vikundi vya wawili ama watatu, jibu maswali haya: Unaamini kukiri mara kwa mara kwa dhambi zako kutakuleta karibu na Mungu?

……

Kwa nini? ……

……..

……..

b) Sasa muulize Yesu kama kuna dhambi yoyote unahitaji kuileta mbele zake. Unaweza ukitaka kuziandika kwa karatasi tofauti.

c) Shiriki na wenzako **(ukiweza)** dhambi unazozikiri **(Yakobo 5:16).** Kama unang'ang'ana na maeneo ya kusameheana **(Mwingine ama wewe),** waweza kuwauliza wengine wakuombee neema ya Mungu ili usamehe.

d) Muombeane, mkiwekania mikono na kuhudumiana upendo wake na msamaha.

YESU KRISTO- MTAZAMO WA MAOMBI

Kusikiza ajenda yake, sio yetu!

MTAZAMO WA MAOMBI

Mnamo mwezi wa nane 1996, Mkutano wa siku nne wa maombi wa wachungaji na wahudumu ulifanywa. Wachungaji thelathini na watano kutoka Toowoomba walikutanika kwa siku nne za maombi na sifa, pakiwa na washika dau wawili, mchungaji kutoka Melbourne na mchungaji kutoka kwa muondoko wa mkutanao wa maombi U.S.A. Makanisa kumi na manane kutoka madhehebu tisa pamoja na wanafunzi na vijana wahuduma waliwakirishwa. Mkutana huo ulikuwa wa maombi na sifa na kuingiana kwa ushirika.

Mkutano uliendelea vizuri kwa sababu ya mambo mawili yalioonekana

1. Kikundi cha waamini kutoka makanisa katika Toowoomba walikuwa wakiomba usiku na mchana kwa sababu ya mkutano huo.
2. Kila mkutano wa maombi ulianza katika mtazamo mpwa wa Bwana Yesu Kristo.

Hapakuwa na yeyote aliyekuwa na shinda ya kumtazama Yesu, tulimpa sifa na shukrani na pia kama vile tulielekezwa, kuyaombea maeneo tofauti. Muda mkubwa ulipatianwa kwa wachungaji waliohudhuria waje kwa Yesu kwa toba na kukiri. Sifa na shukrani zilifuata kwa Bwana.Wachungaji walifurahia kuwa pamoja katika uwepo wa Bwana. Mazao mengi mazuri yamefuata katika maisha ya kanisa Toowoomba kama matokeo tangu mkutano huo ufanyike. Tangu mkutano huo, uhuthuliaji wa maombi ya kila ijumaa ya wachungaji umekuwa na wachungaji 20 na 30.

FUNGUO ZA MAOMBI YA KIKUNDI YENYE USHINDI

Kiongozi/Mwelekezi

Kuwa na mwelekezi atakayepatiana uongozi unaohitajika. Njia ya uongozi ni ile ya mtumishi wa kweli ambaye moyo wake uko kwa washiriki wengine katika kikundi cha maombi, pia ambaye ana maono safi ya maombi na wajibu katika kumtumikia Bwana.

Sifa

Kila mara anza na himizo ya kumtazama Yesu na ulete sifa na shukrani kwa Mungu kupitia kwa Bwana wetu.

Wakati huu unaweza kuhusisha pambio zinazofaa, nyimbo au tenzi. Hii inaingia vizuri, wakati mshiriki mmoja anaanza wimbo kwa taratibu. elewa kwamba wakati mwingine watu wanabebwa na nyimbo wanazopenda na sio kuambatana na mwongozo wa Roho Mtakatifu.

Kukiri dhambi na kutubu

Wakati huu wa mtazamo waweza kuhusisha kukiri na kutubu. Mwelekeo kutoka maandiko kama ***Warumi 12:1-2)*** ni ya msaada tosha kwa watu wanaotaka kuja kwenye uwepo wa Mungu.

Warumi 12:1-2 yasem je?

Waweza kuitumia namna gani katika mkutano wa maombi***?***

Kumngojea Bwana

Sura ya pili ya mkutano wa maombi ni kumuuliza Bwana lile anataka uombee. Himiza wahusika kusikiliza Roho Mtakatifu na kushiriki mawazo na mambo ambayo yanakuja kwa mawazo yao. Kwa jumla mwelekeo sawa utatokea katika wakati huu wa mazungumzo. Kwa msaada wa kiongozi makubaliano yatafikiwa na makubaliano ya mahali pa kuanzia.

Wakati huu, shiriki ombi lolote lililoletwa kwa mkutano. Yanaweza kuwa yameandikwa; ni ya muhimu yawe yameadikwa. Mkubaliane kwamba mahitaji yataombewa mkutano uedeleapo kama Roho atakavyoelekeza na kushawishi.

Sehemu hii yaweza kuhusisha mazungumzo lakini kushiriki kuwe na mtazamo na mwendelee na maombi haraka iwezekanavyo.

Makubaliano

Anza kuomba kuhusu mambo ama hoja mliokubaliana. Ni ya muhimu kumuuliza mtu aliyelitaja jambo kuongoza katika ombi. Himiza wengine waombe kwa makubaliano kama vile wataelekezwa. Himiza iwe kwa kifupi, ilenge ombi ili wengine waombe kwa wepesi wakithibitisha na kuunga maombi. Wakati mwingine maombi marefu yanaongozwa na Roho lakini jizuie na maombi marefu ambayo inabeba mzigo na hoja. Kila mzigo unahitaji kuombewa mpaka amani ya Roho Mtakatifu iwafikie wale walio katika kikundi; kisha ni wakati wa kuombea jambo lingine.

Kuelekezwa na Roho

Utajuaje wakati wa kuendelea?

Ni sawa kusimama na kuuliza na kuongea?

Kwa jumla Mungu ataelekeza mtazamo wa maombi na wahusika wafahamu kwamba wameondoka na wana amani katika jambo hilo. Wakati mwingine ambi moja laweza kushughulikia jambo fulani lililo katika mengine yajayo. Ni ya furaha kuwa kwa kikundi cha maombi ambacho kinaanza kufanya kazi ndani ya Roho Mtakatifu kwa kuwa wahusika wanahisi mwongozo wa Roho Mtakatifu.

Vipawa

Iwe wazi kwa huduma ya Roho Mtakatifu kupitia vipawa wakati wa maombi. Mara kwa mara Bwana atapeana mwelekeo ama thibitisho kupitia vipawa vya kuona (maono/picha) ama kusikia(neno la hekima, maarifa ama unabii) ndani ya Roho, ama kupitia maandiko.

Kutazama Nyuma

Ni nini kinatendeka wakati bidii ya maombi inakosa ama ionekane hakuna mzigo mzito wa jambo la mtazamo wa maombi? Kila mara iwe tayari kutazama nyuma kwa kusimama uone wengine wanahisi nini; iwe wazi kwa sifa na ibada kwa Mungu; pengine umeruka wakati muhimu wa kutubu na kukiri.

Maombi yanahitajika wakati wa taarifa ya 6:00 jioni

Tom White alikuwa akifundisha katika washa katika Toowoomba mwaka wa 1976. Alishiriki vile BWANA alibadirisha hari yake ya kutizama taarifa za 6:00 jioni. Badala ya kuhuzunishwa na habari za ulimwengu na za mjini, Mungu alimuonyesha kufanya maombezi huku akisikiza. Bwana ametupa changamoto kila mara tubariki katika maombi, haswa viongozi wetu wa kisiasa,

na tujizuie kuwalaani kupitia maneno ambayo yako kinyume kwa maneno na nia. Kama vile tumejifunza kuombea mahitaji ya taifa na mji mbele za Mungu, kuwaombea viongozi wetu kwa majina, tumeshuhudia jawabu za ajabu kwa maombi katika kisiasa katika taifa na maeneo mengine.
Iwe wazi kwa kikundi chako cha maombi kukanyanga kwa imani na kuombea mambo *"**makubwa"***na vile vile shughuli za kanisa; mahitaji ya kijamii na mambo mengine yanayohusiana na kanisa. Mungu analiita kanisa lake liombee ufalme wake hapa duniani, kuyafahamu mapenzi yake na kuomba yatendeke kwa shughuli za watu**.**

Ushuhuda / yaliyotendeka.
Ni vyema mwelekezi awe kiongozi. Mikutano ya maombi yaitanwa na kuhudhuriwa kwa kusudi la maombi, sio shuhuda ama mafundisho ya Biblia. Hata hivyo kutakuwa na jawabu za maombi na watu watataka kushuhudia. Hii ni ya kujenga imani kwa wote walioko. Zuia kinyume na maongeo yatakayo watoa watu kwenye mtazamo.

Jambo la kujadiliana wawili kwa wawili
Katika hali ya maombi ya kikundi, unafikiri ni wakati upi uliofaa wakuleta maombi ya kibinafsi? Kwa nini?

ZOEZI LA SEHEMU YA PILI

Mjigawe katika vikundi vya watano au sita. Tambueni mahitaji moja mpaka tatu na mjizoeze kuyaombea kama vile tumeonyeshwa katika sehemu hii.

SIFA KATIKA MAOMBI

Lengo: Kufundisha juu ya sifa na kuongoza juu ya sifa yenye mtazamo; kujifunza juu ya kumngonjea Roha Mtakatifu, kusikiza zaidi, kumruhusu yeye akuelekeze na aachilie mwelekeo wa kweli.

Tumehimizwa kuingia lango lake na shukrani, nyua zake na sifa. Mungu hudumu (hukaa) katika sifa za watu wake. Mungu ameinuliwa katika sifa za Israeli [***Zaburi 22:3].*** Tunaposifu, Roho Mtakatifu anatuachilia kwenye uwepo wa Mungu. Tunaelewa zaidi juu ya Bwana na utukufu wake! Sifa ni njia yenye nguvu ya kutambua Bwana na utukufu wa mbinguni! Sifa hufungua mlango kwa Mfalme wa wafalme!

Nguvu za giza hutoweka wakati tunamsifu na kumuabudu Mungu! Kupitia kuingia ndani ya sifa tunanyenyekea kwa Bwana na kukiri neno lake. Hawa wanamshinda yule mwovu [**Yakobo 4:7].** Sifa kwa Mungu ni sehemu ya muhimu ya maombi na ina wajibu maalumu katika maeneo ya vita vya kiroho, kushinda kugandamizwa. Juzi, nilikua mojawapo wa watu watatu wa kikundi kilicho hudumia mtu aliye shambuliwa na roho mchafu. Pepo alitambuliwa lakini alikuwa anakataa kuondoka. Tulikuwa na watu wengine walioomba nasi lakini haikuwezekana mpaka tulipowauliza kuingia kwa sifa ambapo ushindi ulikuja. Mara tu nguvu za pepo zilivujwa, yule mtu aliweza kukiri dhambi na msamaha na yule pepo akaondoka kwa upole. Kuna utendaji kazi wa neno la ushuhuda tunaponena neno la Mungu katika sifa.

KUTAZAMA SIFA KUPITIA MAANDIKO

Sifa za Mungu ni katika Biblia, lakini sehemu kubwa ni katika zaburi. Maneno kadhaa ya kiebrania yanatumika ambayo yanatafsiriwa “sifa”.

i. ***halal***, neno la msingi: ***kujivuna, kusifu***; halal pia yamaanisha **Kuangaza.** Imetafsiriwa mara 121 kama jina, sifa; mara 18 kama kulinga; mara 8 kama utukufu; mara 12 maneno mengine ya kingereza.

ii. ***yadah*** **NASC, 1981 NO 3034** Msingi wa kale maana yake ***kutupa, rusha***; pia ikimaanisha ***kukiri, sifu, kushukuru, kupatiana sifa.*** **TWOT, 1981 NO 847** Katika matumishi ya kuelekeza sifa kwa Mungu, yamaanisha: kutambua ama kukiri tabia ya Mungu na kazi, pia inaeleza kukuri dhambi na inatumiwa kukiri tabia za mtu mpya. Imetafsiriwa mara 19 kama ***sifa***, lakini mara 70 kama ***shukrani***, mara 16 ***kukiri***, na mara kadha wa kadha **yadah *imetumika kama kutangaza kazi ya* Mungu. TWO 1981 P 364** Sifa ni kukiri kutangaza Mungu ni nani na matendo yake. Yatafsiri mara kwa mara kama ***“shukrani***”, neno hili linahusisha shukrani kama njia ya kusifu.

iii. ***Tehillah,*** NAS.C 1981 NO 8416 Kutoka 1984 (hali) maana ***sifa, nyimbo za sifa;*** imetumika mara 55 kwa mfano wa jina sifa. Neno la Kiebrania lenye msingi halal, ambalo ni msingi wa tehillah, “Yaonyesha kuwa wazi na shukrani za ndani". TWOT,1981 P217) jina lililofanana la kiebrania ni yadah - ***Kupatiana sifa ama shukrani; ranan - kuimba ama kupaza sauti kwa furaha; barak- kubariki ama kusifu; gadal-kutukuza; rum- kuinua; Zamar-kuimba, kucheza, kusifu.***

TUMEAMRIWA KUSIFU
Katika Zaburi, wito wa sifa sana sana huja kama ujumbe kwa mfanao wa ***Zaburi 100:1 "Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote".***

Sifa zahitajika katika maisha ya watu wa Mungu. Mungu anatambuliwa na utimilifu wake kuthibitisha na kutangazwa.

Sifa zastahili kutolewa kwa nia ya kujifurahisha na kufurahi *(**Wafilipi 4:4).*** Kuamini na furaha zinaingiana ***(Zaburi 27:13).***

Wito wa sifa ni kwa wingi, kutuonnyesha ibada ni ya kusanyiko. Sifa mara kwa mara zahusisha kuimba pamoja na kutumia vyombo vya mziki (***Zaburi 144:9b, 33:2, 71:22).***

Tazama maandiko haya na uandike kitendo cha sifa:

Zaburi 105:2b ---------- Zaburi 9:2 ---------- Zaburi 9:11----------

Zaburi 105:2a ---------- (Zaburi 5:11)

Zaburi 149:3 ---------- (Zaburi 150:4, 2 Samueli 6:14)

Zaburi 63:4 ---------- (Zaburi 141:2)

Zaburi 47:1 ---------- (Zaburi 98:8, Ayubu 27:23)

Zaburi 71:23 ---------- (Zaburi 32:11)

Zaburi 96:1 ---------- (Zaburi 40:3. 33:3, 98:1, 144:9a Isaya 42:10)

Andiko linahimiza maamuzi ambayo mtu binafsi atachukua kumsifu Mungu ***(Hab 3:17 -18)*** yesema, "***Walakini nitamfurahia BWANA, nitamshangilia Mungu wa wokovu wangu***". ***Zaburi 103:1* "*Ee nafsi yangu, umuhimidi BWANA. Naam, vyote vilivyo ndani yangu Vilihimidi jina lake takatifu***". Lazima tujieleze kwa maneno – sifa ni za kuzungumza. Kumuinua Bwana mbele ya watu na matendo yake ni ya muhimu sana kuonyesha maisha yenyewe. ***Zaburi 150:6*** "***Kila mwenye pumzi na amsifu BWANA. Halleluya***".

Mungu ndiye wa muhimu sana na mtazamo wa ibada ya kweli. Yeye hawezi kutenganishwa na sifa. kuishi kwa mwanadamu na sifa za Mungu wa kweli zina uhusiano wa karibu sana. ***"…Wote wenye mwili na walihimidi jina lake takatifu milele na milele***" ***(Zaburi 145:21).*** Kama watu hawatamsifu Bwana, atayainua mawe ili yamsifu *(**Luka 19:40).*** Maisha ya utajiri mtimilifu wa mwanadamu yanatoa sifa za kuendelea. Kuendelea kujisifu (kujitukuza) kwa mwanadamu kwastahili kuwa katika Mungu. ***Zaburi 28:6-7 "Na ahimidiwe BWANA. maana ameisikia sauti ya dua yangu; BWANA ni nguvu zangu na ngao yangu. Moyo wangu umemtumaini, Nami nimesaidiwa; Basi, moyo wangu unashangilia, Na kwa wimbo wangu nitamshukuru".***

Je, moyo wako unashangilia kwa furaha? Utamshukuru Mungu kwa nini***?***

Sifa za Mungu zitajaza ulimwengu. Mungu anatangaza hataruhusu mwingine achukue sifa zake. Sifa za Mungu **zitatangazwa (*Zaburi 29:1-11);* Zahesabiwa (*Zaburi 78);*** na daima **zitaongezeka** (***Zaburi 148 na 150*).**

Sifa zake zaunganishwa na matendo yake ya ukombozi katika historia kwa niaba ya watu wake (***Zaburi 78:105)***, lakini sifa zaweza kutukomboa sasa (***Zaburi 32:7).***

Mungu huadhimishwa kwa sifa (Zaburi 69:30). Mungu aliye Bwana ndiye mtazamo wa sifa. Mataifa yote **(Zaburi 45:17)** yamsifu Mungu; wafalme wote **(*Zaburi 138:4)*** na mbingu **(*Zaburi 89:5*)!**

SIFA KATIKA AGANO JIPYA

Waebrania 13:15:* "*Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la mdomo iliungamayo jina lake".

1 Petro 2:5: "***Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazo kubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo***".

1 Petro 1:8: Petro anazungumza kuhusu "***kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu***".

Luka 1:46: Maria alimsifu Mungu: "***Moyo wangu wamuadhimisha Bwana. Na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu***"

Yesu "***alipakwa mafuta ya furaha***" (***Waebrania 1:9)*** na ***kumsifu Mungu*** (***Mathayo 11:25-27).*** Yesu aliendelea kuzungumza juu ya Baba yake na kumpa yeye heshima na utukufu, daima akimtambua kama chanzo cha aliyo yafundisha na aliye fanya miujiza kupitia Yesu.

Maisha yetu yapaswa kumsifu mungu

Kama vile waamini wa Agano Jipya waliishi imani yao, wakadumu katika upendo, kukua katika maarifa ya kweli na kupambanua, wakijazwa na tunda la haki litokanalo na Yesu Kristo, Mungu alipokea utukufu na sifa **(*Wafilipi 1:9-11).*** Katika **(*Waefeso 1:6)*** kuchaguliwa kwetu ndani ya Kristo na kuiweka hatima yetu tufanywe wana ni "***Kwa sifa ya utukufu wa neema yake".*** Pamoja na hayo, akatutia muhuli kwa Roho Mtakatifu wa ahadi kama alabuni ya urithi wetu ili tupokee ukombozi wa Mungu kamili, ambao ni "***kwa sifa na utukufu wake***" (***Aya 13-14***). Baba anatukuzwa wakati sisi kama wanafunzi wake tunazaa matunda mengi kwa maombi **(*Yohana 15:7-8)***. Yesu aliuliza Baba yake auweke utukufu wake kwa waanini, utukufu ambao yeye alipokea kutoka kwa Baba **(*Yohana 17:22).***

Kama Mariamu aliye msifu Mungu kwa makubwa aliyomtendea ***(Luka 1:46-55),*** Vivyo hivyo nasi tumsifu Mungu kwa makubwa aliyoyatenda na anaendelea kuyatenda kwetu. Sifa zinahusisha kuyatazama matendo ya historia ya wokovu ambayo Mungu ametenda na baraka ambazo zinatiririka kutoka matendo ya historia yaliyopita, vile vile yale mambo anayoyatenda katika maisha Yetu na ulimwenguni wote sasa.

Je, "historia" yako ni ipi ya wokovu?

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Maombi na nyimbo za sifa

Maombi na nyimbo za sifa zapatikana kote katika Biblia**.**

- ***Yakobo*** alimsifu Mungu katika ***Mwanzo 48:15-16,*** alipo wabariki wana wa Yusufu.
- ***Musa*** na wana wa Israeli waliimba nyimbo za sifa kwa Mungu (***Kutoka 15),*** na Miriamu na wanawake walimchezea na vyombo waliposherehekea ukombozi kutoka misiri na ushindi wa bahari ya Shamu.
- ***Hana*** alimsifu na kumuinua Mungu kwa maombi (***1Samueli 2:1-10)***. Alikuwa amepokea ombi lake la hitaji la ndani.
- ***Daudi*** anakumbukwa kama muandishi mzuri wa Zaburi wa Israeli. Katika ***2 Samueli 22,*** aliziimba sifa za Bwana. ***Sulemani*** alimsifu Mungu kwenye umati alipoitakasa Hekaru katika ***1 Wafalme 8.***
- Waandishi wengi wa Zaburi walifika kiwango cha juu katika sifa. Katika vitabu vya manabii, kuna sehemu nyingi zinazungumzia utukufu wa Mungu na sifa. Nyaraka za Paulo, Petro na Yuda wana maelezo ya ajabu ya sifa waandishi wakitafuta kuonyesha ajabu ya upendo na neema na utukufu.
- ***Warumi 16:25-27; Waefeso 3:20-21; 1 Timotheo 1:17; 1 petro 1:3; Yuda 24:-25.***
- Kitabu cha ***Ufunuo 1: 4-5*** chafika kiwango cha juu ya vyote Yohana anapoonyesha sifa na ibada mbinguni. Halleluya!

HITIMISHO

Kutoka mafundisho ya sifa katika maandiko twaweza kusema sifa ni njia ya uzima. Sifa ni zaidi ya kifaa kinachotumiwa kuja kwenye uwepo wa Mungu. Ni kitu cha muhimu sana cha kuonyesha uhusiano wetu na yeye.
Hebu tuwe watu wa kumsifu. Hebu tuwe na mtazamo wa mikutano ya maombi katika sifa**.**

ZOEZI YA SEHEMU YA TATU

Tumia mda sasa kumsifu Yesu na Baba kupitia kuwezeshwa na Roho Mtakatifu kwa wokovu wako na mambo ambayo yanafanya moyo wako ushangilie.

VIPAWA VYA ROHO MTAKATIFU NA MAOMBI

Jambo la kuhuzunisha, ni kwamba kwa wengi maombi yamekuwa **nidhamu** badala ya **fahari.** Mikutano ya maombi haijajulikana sana kwa wengi. Kwa wengi, mikutano ya maombi haijawanjenga, ikikosa nguvu, ikikosa mwelekeo na makubaliano, na ikikosa shuhuda za maombi yaliyojibiwa.

Wakati Paulo alienda Efeso na akakutana na wanafunzi huko, lazima alihisi jambo la muhimu linakosekana katika ushirika kwa maana aliuliza, "**Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"** Paulo alitambua kwa haraka ukosefu wa uwepo wake, pengine kwa sababu ya ukosefu wa imani iliyo hai na ukosefu wa vipawa vya Roho Mtakatifu**.**

ROHO MTAKATIFU NA YESU

Matahayo 3:16: "Na yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake".

Luka 4:1: "Na Yesu, hali amejaa Roho Mtakatifu…"

Luka 4:14: "Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akaenda Galilaya…"

Matendo 10:38: "Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu; naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na kuponya wote walioonewa na ibilisi; kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye".

Yesu hakuanza huduma yake mpaka alipojazwa, ama alipopokea upako wa, Roho Mtakatifu. Alikuwa tayari "***amezaliwa na Roho"*** kwa kuwa kupatikana kwake ilikuwa ni kwa Roho Mtakatifu ***(Luka 1:35)***

ROHO MTAKATIFU NA MWAMINI

Mungu aliahidi kupitia nabii Yoeli, "***nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili***" ***(Yoeli 2:28*)**.

Yesu pia aliahidi Roho Mtakatifu atakuja kwa nguvu. ***Mdo 1:8: "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu…".*** Alisema katika ***Mdo 1:5*** "***Mtabatizwa katika Roho Mtakatifu".***

Katika injili zote, Yohana amuona Yesu kama yule abatizaye kwa Roho Mtakatifu ***(Mathayo 3:11, Mariko 1:8, Luka 3:16, Yohana 1:33).***

SIKU YA KUZALIWA KWA KANISA

Kabla ya kuja kwake Roho Mtakatifu siku ya Pentekote, wanafunzi hawakuwa na nguvu ndani yao. Yesu alipo twaliwa, waliogopa. Tazama tofauti ambayo Roho Mtakatifu alifanya siku ya Pentekote.

Mdo 2:4 "Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyo wajalia kutamka".

Katika ***aya 38,*** Petro anatangaza ***"Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu". Mdo 2:39: "Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie".*** Kipawa cha Roho Mtakatifu hakikuwa chao peke yao.

NI NANI AWEZAYE KUPOKEA ROHO MTAKATIFU?

"*Wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu!" (Mdo 2:39)*

Kama tumezaliwa na Roho wa Mungu, lazima tuwe na Roho ndani yetu. ***1 Wakorintho 12:3 "Wala hawezi mtu kusema, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu".*** Kwa nini baadhi ya waamini harisi wamesema vipawa vya Roho Mtakatifu sio vya wakati huu? Kama tumepokea Roho Mtakatifu kama vile Yesu aliahidi, je amebadilika kutoka kwa utu wa Mungu kama alivyo wakirishwa katika Bibilia? Yesu alisema tutapokea nguvu mpya akitujilia Roho Mtakatifu ***(Mdo 1:8);*** Alisema ishara za miujiza zitawafuata waaminio **(*Mariko 16:17-20).***

Wakati Petro na Yohana waliteremka Samaria na kuwawekea waamini wapya mkono, "***walikuwa wanapokea Roho Mtakatifu***" **(Mdo 8:14-18).** Waamini wapya waliobatizwa kule Efeso, "***Wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri***" **(Mdo 19:1-7)** wakati Paulo aliwawekea mikono na Roho Mtakatifu akaja juu yao**.**

BAADHI YA VIPAWA VINGINE VYA ROHO MTAKATIFU NI VIPI?

1 Wakorintho 12:4-11 yaorothesha vipawa kenda vya Roho (***neno la hekima; neno la maarifa; unabii; ndimi; kutafsiri kwa ndimi; imani; miujiza; vipawa vya uponyaji; kupambanua maroho).*** Baadhi ya vipawa hizi zinafanya kazi na zina nguvu zikipatianwa na Roho Mtakatifu katika mikutano ya maombi. Kuna vipawa vingine vya Roho Mtakatifu katika Agano Jipya, lakini hizi haswa zimeelezewa katika kifungu hiki cha mikutano ya kanisa na baadhi yazo zinatumika katika mikutano ya maombi.

Neno la hekima laelezwa vyema kama kuzijua njia za Mungu ama mapenzi yake katika hali Fulani; ama, uweza wa kutumia neno la Mungu katika hali.

Neno la maarifa ni kuonyesha jambo ama hekima kuhusu hali ambayo Roho anapatiana, ambalo halingejulikana kikawaida.

Unabii ni kutangaza neno la Mungu. Ni kuyaeleza mapenzi ya Mungu kwa wakati fulani au hali. Unabii ni kujenga, kufariji na kutia moyo (1 Wakorintho 14:3). **Kutafsiri ndimi** ni sawa na unabii**.** Unabii unaweza kuhusisha baadhi ya zile za kwanza mbili (neno la hekima, na neno la maarifa). Watu hupokea vipawa hivi kwa neno ama jia ya kufikiri, ama kupitia kuelekezwa kwa maandiko, hivyo ni, kuwa na aya ambayo inafaa na kueleza, ama kwa mfano wa picha ama maono, ambayo yanaweza kugawanywa/kushiriki. Wakati mwingine neno ama picha zahitaji kutafsiriwa kama vile ujumbe katika ndimi wahitaji kutafsiriwa.

Kipawa cha imani ni spesheli ama imani spesheli kwa hitaji spesheli ambayo Roho anatamani kukutana nayo. Mtu anayefanyisha kazi kipawa hiki anathihirisha imani ambayo haikati tamaa mpaka nguvu za Mungu zipenye.

Miujiza ni kazi za nguvu. Mambo yasio ya kawaida yanatekelezwa na mwamini katika kuuitikia msukumo wa Roho Mtakatifu.

Vipawa vya uponyaji (maneno yote mawili ni katika wingi katika kiyunani). Mungu hajapungukiwa. Maradhi yote na magonjwa yaweza kuponywa.

Kupambanua maroho ni kipawa cha muhimu sana kwa maombi yanayo fanya kazi. Kwa hali fulani Roho anapatiana kupambanua roho chafu ambazo zastahili kukemewa.

VIPAWA VYAFANYA KAZI NAMNA GANI KATIKA MKUTANO WA MAOMBI?
Vipawa vinaleta ***uthibitisho,*** kwa kuleta ushahidi wa pili au wa tatu kwa maombi ya mtu.
Kupokea ushahidi wa Roho kupitia kipawa cha hekima, maarifa ama unabii, ndimi na utafsiri, ama kupambanua kwa roho, zaelekeza kwa maombi ya kukubaliana, inahimiza imani ya wenye kuomba katika vikundi vya maombi, na kuhakikisha Mungu anasikia na kujibu kwa njia nyingi.

NI NANI AWEZAYE KUFANYA KAZI KWA VIPAWA VYA ROHO?
Kama wengi walivyo "***Tumbuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu***" **(*Mdo 2:38-39).*** Katika *(1* ***wakorintho 12:1-3),*** Paulo anapendekeza ya kwamba kila mtu ambaye anaweza kusema, "***Yesu ni Bwana",*** amepokea Roho Mtakatifu na kwa hivyo hastahili kupuuza vipawa vyake***.***

VIPAWA VYAMLETEA MUNGU UTUKUFU

Kwa mfano, kukiwa kuna kipawa cha nabii na mtu asiyeamini ama asiyefahamu yuko katika mkutano, yeye ataanguka chini na kuabudu; "***Hakika Mungu yu miongoni mwenu***" ***(1Wakorintho 14:24-25).*** Kama mtu ameponywa watampa Mungu sifa. Karibuni tulikuwa tukihudumu kwa mji usiku na kufanya mkutano wa nje wa maombi mchana. siku ya tatu kikundi kipya cha watu kikaja kwa mkutano wakisema, "tulisikia kwamba kuthihirishwa kwa Mungu kuu miongoni mwenu". Utukufu wa Mungu ulithihirika na neno likaenea.

HITIMISHO

Twahitaji tujazwe na Roho Mtakatifu, ***Waefeso 5:18-19.*** Hii ni pamoja na kujazwa na maarifa inayokua ya neno lake kupitia zaburi na tenzi na nyimbo za kiroho**.** Roho Mtakatifu anapenda kuachilia vipawa vyake kuujenga mwili wa Kristo. Anapenda kujaza nguvu watu wa Mungu ili washinde adui na kushuhudia kwa nguvu kwa waliopotea. Maombi bila vipawa vya Roho Mtakatifu na nguvu ni kazi ngumu na haiwezi kufanya kazi kama maombi ambayo yanaelekezwa na Mungu Roho Mtakatifu mwenyewe.

Zoezi la Sehemu ya nne

1. ***Tumia muda peke yako ukiorodhesha vipawa vya Roho Mtakatifu ambavyo unafikiri Roho Mtakatifu amehudumu kupitia wewe.***
2. ***Tafakari katika maombi, ukimtafuta Mungu kwa jawabu. unaweza penda kutumia Biblia yako.***
3. ***Katika vikundi vya watano au sita, omba kuwezeshwa na Roho Mtakatifu kupitia kuwekewa mikono. (Kama kuna neno au maono, yashiriki wakati huu).***

Tafadhali kumbuka: Kiongozi anaweza kuamua umuhimu wa kutouliza/ kutoshiriki jawabu za sehemu ya (1) ya zoezi kuhusu vipawa kabla ya muda huu wa maombi, ili kusiwe na kuiga.
waweza kupenda kuandika neno lolote/maono uliyopokea kwa matumizi ya baadaye/uthibitisho.

SILAHA ZA MUNGU

UTANGULIZI

Maandiko katika kitabu cha ***Waefeso 6:10-20*** ni ya muhimu sana na yanatakikana kueleweka na kutumika. Paulo anaongea kuhusu upinzani wa kiroho wa watu wa Mungu ambayo ni ngumu sana, yakupotoa na nguvu ambazo twatakiwa kujifahamisha. Anatujulisha ufahamu wa roho wa dunia ambayo inatambulika na watu wengi wa siku hizi. Kisha anatuelekeza jinsi ya kuvaa silaha za Mungu ili tuweze kujikinga kiroho na kuondoka kwenda kupinga na kuondoa upinzani.

MWE HODARI KATIKA BWANA

Efe 6 :10 "***Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake".***

Baadhi ya maandiko yanathibitisha himizo hii kuwa hodari katika Bwana.

Yoshua 1:7: uwe hodari na ushujaa mwingi;
Yoshua 1:9: Uwe hodari na moyo wa ushujaa;
Zaburi 27:14: Umngojee Bwana, uwe hodari;
Waefeso 3:16: mfanywe imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani;
2 Timothio 2:1: uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu;
1Wakorintho 16:13: Kesheni, simameni imara katika Imani, fanyeni kiume, mkawe hodari.
Hizi ***nguvu za uweza*** ni 'uwezo ambao Mungu ameweka ndani yako kupitia upako'.

Ni silaha za Mungu

Efe 6:11: "*vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za shetani".*

Ni silaha za Mungu na sehemu na silaha zimetajwa katika baadhi ya maandiko. Paulo anaiita "***silaha ya nuru***" **Warumi 13:12** na anasema twastahili tuzivike kama wana wa nuru. Tumekombolewa kutoka kwa giza (**Wakolosai 1:13).**

Isaya 59:17a: "Akajivika haki kama deraya kifuani, na chepeo cha wokovu kichwani pake".
Ufunuo 1:16: "Na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake" Ufu 2:12
Ufunuo 2:16: "nami nitafanya vita juu yao kwa huo upanga wa kinywa changu".
Ufunuo 19:15: Na kwa upanga, Yesu***, "atawapiga mataifa kwa huo".***
Isaya 11:5: "Na haki itakuwa mshipi wa viuno vyake, na uaminifu mshipi wa kujifungia".
Isaya 52:7: "Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema, Yeye aitangazaye amani, aletaye habari njema ya mambo mema, yeye autangazaye wokovu, auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki.
Mwanzo 15:1: Mungu mwenyewe ndiye ngao yetu.
Zaburi 7:10-13: "Ngao yangu ina Mungu, awaokoaye wanyofu wa moyo".
Zaburi 7:12b: "Ameupinda uta wake na kuuweka tayari"

Kusimama kinyume cha hila ya ibilisi

Yatupasa kusimama kinyume cha hila ya ibilisi (**hila**) yamaanisa udanganyifu neno lile pia latumika katika ***Waefeso 4:14*** kama ujanja au undanganyifu.

Adui ni nani?

Waefeso 6:12: "*Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa ngiza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho".*

Aya hii inatupa sababu ambayo inatufanya kuvaa silaha za Mungu. Wakristo wengi wamechagua kupuuza uhakika wa nguvu ambazo zinapinga kanisa, wakindanganya ulimwengu na kusababisha madhara kwa wakristo na wasio wakristo. Wengine wameenda mbali sana na kufundisha kwamba shetani si kiumbe halisi. Matokeo ni kwamba, tumepungukiwa na mafundisho kuhusu silaha za Mungu. Kushindana kwetu si kwa watu au mashirika; kama wakristo, sio watu ambao ni adui zetu. Tumeulizwa kuwapenda adui zetu. Vita vyetu ni kinyume cha maadui wa kiroho katika ***aya 12.*** Mpinzani wetu ni shetani na anang'ang'ana kusukuma watu wa Mungu ***1 Petro 5:8***

Siku ya uovu

Waefeso 6:13: "*kwa sababu hiyo, twaeni silaha zote za Mungu, mpata kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama."*

Pengine umekuwa na vita kabisa! Yawezekana unajua vile ilivyo wakati kila kitu hakiendi sawa; wakati ulimwengu wako umeanguka pasipo kutarajia. Ulisimama vipi? Imani yako ilikuwa imara? Ulikuwa pahali pa salama?
Wafikiri utafanya nini ukikumbana na vita wakati mwingine?

MSHIPI WA KWELI

Waefeso 6:14: *"**Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunononi, na kuvaa dirii ya haki kifuani".***

Luka 12:35: "Viuno vyenu na viwe vimefungwa, na taa zenu ziwe zinawaka" "***viuno vyenu na vifungwe", "viuno vyenu vikiwa vimefungwa". "mvikwe mavazi tayari kuhudumu***".

1 Petro 1:13: "kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi; mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo".
"vifunge viuno vyako kwa matendo".

Yesu Kristo ni kweli na neno lake ni kweli. Mungu anatamani ukweli katika ***utu wa ndani Zaburi 51: 6.*** Hebu ndio yako iwe ndio na la yako iwe la!
Mshipi wa kweli hufunika viuno. Hii inajumuisha utu wetu (utu wetu wa ndani) ***Yohana 7:38.*** Kuna kufunikwa kwa tabia katika maisha yetu tunapo zitoa sehemu zetu za mwili kwa Bwana.
Kuvaa mshipi wa kweli ni kujipatiana kwa Bwana na ukweli wa neno lake. Mtu avaaye mshipi wa kweli hataongea ama kutenda kimakusudi kinyume cha mapenzi ya Mungu, yalioelezwa katika maandiko. Ukweli pia lazima uwe katika mawazo yetu; yatupasa kushawishiwa na ukweli wa neno la Mungu.

DIRII YA HAKI

Waefeso 6:14b: "Na kuvaa dirii kifuani".

1 Wakorintho 1:30: Yesu Kristo amefanyika haki yetu kutoka kwa Mungu.

2 Wakorintho 5:21: Mungu alimfanya Yesu asiyejua dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu kwa ajili yake**.**

Haki hii inapatikana kwa Mungu kwa msingi wa imani ndani ya Yesu Kristo (***Wafilipi 3:9).*** Kifo chake cha kupatanisha kupitia kumwagika kwa damu huondoa dhambi zetu. Dirii hufunika kifua na hivyo moyo. Yesu alisema ni kutoka kwa moyo ambapo aina zote za dhambi hutoka. Tunakuja kwa Mungu tukikiri dhambi zetu na kupokea utakaso wake kutoka kwa mambo yote yasio ya haki. Dirii **hulinda mioyo yetu** kisha ikituweka karibu na Mungu, Roho wake Mtakatifu akidumu ndani.

VIATU VYA INJILI YA AMANI

Waefeso 6:15: "*Na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa injili ya amani".*
Amani inawezaje kuwa sehemu ya silaha za kiroho?
Isaya 52:7 yazungumzia kupendeza kwa miguu yake aletaye injili. Paulo alitumia aya hii katika ***Warumi 10*** kuonyesha **wahubiri wa injili.** Injili ni ujumbe wa amani; "***amani duniani kwa wale wanaotenda mapenzi yake".*** Imani ndani ya Yesu Kristo huleta amani na Mungu (***Warumi 5:1).*** Fahamu ya kwamba mara kwa mara Yesu alipowaponya watu angewaambia "endeni kwa amani; imani yako imekuponya", ama msemo kama huo.

Yesu ndiye Mfalme wa Amani: alisema, "***Amani Yangu ninawaachia, amani yangu ninawapa" Yohana 14:27. Yakobo 3:17*** yasema hekima ya Mungu ni kupenda amani, na kwamba mbegu ambayo matunda yake ni haki hupandwa kwa amani na wale wanaofanya amani (**3:18). "*Heri wapatanishi; maana hao wataitwa wana wa Mungu" Mathayo 5:9.***

NGAO YA IMANI

Waefeso 6:16: "*Zaidi ya yote mkitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu".*
1 Wathesalonika 5:8: "hali tukijivika kifuani imani na upendo, na chepeo yetu iwe tumaini la wokovu".
Mwanzo 15:1: Mungu ni ngao yetu***.***
Waebrania 11:1: "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasioonekana".
Tunapata wapi imani hii? ***Warumi 10:17*** yasema nini?
Imani huja kwa kusikia ujumbe, na ujumbe husikika kupitia neno (neno lililonenwa) lake Kristo. Mungu hutunenea. Tunapo sikia na kutii, imani inafanyiwa kazi. Ni kusikia kwa neno lake ambayo huleta uhakikisho wa hiyo imani.
Je kukiri kuna umuhimu kwa kuamini kwenye imani?
Imani lazima, iwe kuamini kutoka kwa moyo. Paulo anafundisha katika ***Warumi 10:8***, "***Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo".***
Aya 9: "kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka".
Aya 10: "kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu" (matokeo yakiwa haki***).***

Shaka **(**mishale ya adui) zaweza kuja kwa mawazo yako lakini kama imani imeingia ndani ya moyo wako, imani kama ngao, unaweza kukiri kile ambacho unaamini ndani ya moyo wako na ujengwe katika uaminicho. Hali hii ya kukiri imani katika Yesu Kristo kutoka kwa moyo inajenga mawazo ya mtu pia. Sifa ni njia ya kueleza ambacho tunaamini. Kwa ufanisi, tunainua

ngao ya imani kupitia sifa. Mishale ya shetani pia inaongea juu ya mambo yaliyo kinyume ambayo yanachoma mioyo yetu, ikileta majeraha. Mara tu tunapotambua haya yametendeka, kufanyisha imani kazi na njia ya kumfikia Yesu na kuomba uponyaji ambao tunahitaji.

CHEPEO CHA WOKOVU

Waefeso 6:17: "Chukua chepeo ya wokovu…"

Ni ***tumaini la wokovu*** ambayo ni chepeo yetu (***1 Wathesalonike 5:8).*** Mwandishi wa kitabu cha ***Waebrania (6:11)*** anazungumza juu ya uhakika kamili wa tumaini mpaka mwisho. Tumaini hili ***(aya 19***) tunalo, kama nanga ya moyo, tumaini ambalo ni imara na hakika, ambalo linaingia ndani mwa pasia. Tumaini hili huja kwetu kupitia neno na pia tumaini la kweli laleta imani (***Warumi 4:18***).

Chepeo hufunika kichwa na hivyo inamaanisha kufunika mawazo na nia zetu. Tumepokea roho wa mawazo yaliyofanywa upya (***Waefeso 4:23)*** na kupitia Roho wa Mungu, tunaweza kujua mambo ambayo Mungu ametukilimia (***1 Wakorintho 2:12).*** Tunapaswa kuyaweka mawazo yetu kwa mambo yaliyo juu, ambako Kristo ameketi ***Wakolosai 3:1-3.***

Matokeo ya mwisho ya unyenyekevu wetu kwa Mungu na vita vyetu juu ya adui ni "***tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo" (2 Wakorintho 10:5).*** Yoshua aliambiwa "***alitafakari neno mchana na usiku",*** na atafanikiwa (***Yoshua 1:8).*** Mwandishi wa zaburi anatuambia juu ya baraka kwa yule mtu anayejifurahisha katika sheria ya Bwana na kuitafakari mchana na usiku (***Zaburi 1***). Isaya anaahidi amani kamilifu kwake ambaye mawazo yake yameimarika, ambaye tumaini lake ni katika Bwana ***(Isaya 26:3).*** Chukua chepeo cha wokovu: fikiri juu ya Yesu na ambayo ameyatenda.

UPANGA WA ROHO

Waefeso 6:17b "… na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu".

Upanga hapa ni neno la Mungu alilo linena kwetu na ni neno la Mungu lililohuishwa ambalo Yesu alitumia katika ***Mathayo 4*** kuyashinda majaribu ya shetani. Hata hivyo neno la Mungu lililo andikwa linafananishwa na upanga ukatao kuwili (***Waebrania 4:12)*** na kulijua na kulitumia neno lililoandikwa lina nguvu sana pia.

Kumbuka upanga wa Roho ni ***neno la Mungu,*** neno lililohuishwa na neno lililo andikwa. Neno la Mungu kwangu katika hali hii ni gani? Neno la Mungu kwa kanisa langu ni lipi? Upanga ni silaha ambayo sio tu ya kujikinga bali linaweza kutusaidia kupigana vita. Tunaweza kusonga mbele ndani ya Kristo tunapopokea (kusikia) neno lake na kulitii.

MAOMBI

Waefeso 6:18-20 yahimiza sehemu ya msingi ya maombi katika utendaji uliofaulu wa silaha. Mara umuhimu wa maombi katika silaha zote za Mungu haijashirikishwa katika mafundisho katika swala hii.

Kwa watakatifu wote (aya 18)

Twapaswa kuomba katika Roho. Ni upanaga wa Roho anaotupatia kutuelekeza na ni ombi la Roho ambalo litatupatia upenyo. Kuomba ndani ya Roho inafaa katika hali zote, kwa maombi aina zote na dua. Tunapaswa kuwaombea watakatifu wote, tukiwa makini na tukikesha kwa

kusudi lililo imara na kustahimili. Twapaswa kumsihi Mungu kwa watakatifu kwa kuwataja majina na kuwaombea.
Baadhi ya watakatifu unaowaombea mara kwa mara ni wakina nani?
Je una mtu mnayeomba na yeye, ama mtu anayekuombea mara kwa mara? Kama sivyo mbona usiombe sasa ukimuuliza Mungu akupe mtu kama huyo?

Kwa kuhubiri neno (aya 19-20)
Paulo anauliza ombi spesheli kwa huduma ya kuhubiri. Anaomba usememi (lakusema) na ujasiri uo kutoogopa. Mungu anarejesha huduma ya kuhubiri na kufundisha kanisani. Wakati neno linanenwa katika nguvu na mamlaka kanisa linajengeka na ngome za adui zinaharibika. Paulo alikuwa ngerezani alipoandika barua hii. Hatarajii vifungo vyake vimzuie kuhubiri mladi tu msaada wa maombi ni imara.
Je una huduma? Sisi sote tu "mashahidi". Paulo aliuliza "usemi "na "ujasiri" ungemuuliza Mungu nini kwa huduma yako? Usemi? Ujasiri? Fulsa? Hekima? Ubabanuzi? Imani? Nguvu? Ulinzi?

HITIMISHO
Fundisho hili la silaha za Mungu latuelekeza katika hilo lingine la silaha za vita vyetu. Kuna mapatano na makubaliano kati ya mambo haya mawili ya mwendo wa Mkristo.
Ninaomba macho ya ufahamu wetu yafunguliwe na Roho Mtakatifu tunapochukua silaha kimaombi na kujifundisha kutembea ndani yake, tukifunikwa kikamilifu.

ZOEZI LA SEHEMU YA TANO:

Mkifanya kazi katika vikundi vidogo, kimaombi vaeni silaha zaMungu. Anzeni kwa mazungumzo, mkiorodhesha mambo mtakayoombea na kupokea kila sehemu ya silaha. Kila mtu katika vikundi hizo ndogo na aongoze katika maombi, akivaa sehemu ya silaha.

- ***Mshipi wa kweli.***
- ***Dirii ya haki.***
- ***Viatu vya injili ya amani.***
- ***Ngao ya imani.***
- ***Chepeo cha wokovu.***
- ***Upanga wa Roho.***

SILAHA ZA VITA VYETU

Katika kutuelekeza kuhusu vita vya kiroho, Paulo katika (***2 Wakorintho 10:4***) anatwambia kwamba silaha zetu si za mwili (au dunia hii), lakini ni za kiungu zenye nguvu (uweza mbele ya Mungu), kuharibu ngome. Silaha hizi ni zipi ambazo Mungu amepatiana kanisani?

Ufunuo 12:7-10) yatwambia habari ya vita mbinguni kati ya Mikaeli na malaika wake na joka na malaika zake. Shetani alishindwa katika vita na akarushwa ulimwenguni. Yeye ndiye mshitaki wa wapendwa/ wa ndugu, ambaye anawashtaki mchana na usiku. "***Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana –Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa***" ***(aya 11).*** Silaha tatu zenye nguvu ambazo zitamshinda shetani na malaika zake zimeorodheshwa hapa.

- ***Damu ya Mwana – Kondoo;***
- ***Neno la ushuhuda wao;***
- ***Kutopenda maisha yao hata kufa.***

DAMU YA MWANA KONDOO

Sadaka ya mauti ya Yesu ndio mtazamo wa mafundisho ya agano jipya. Yesu alifanya agano jipya ndani ya damu yake: "***kwa maana hii ndiyo damu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi" (Mathayo 26:28). "Na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo****".* Yesu ndiye "***atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake, na kutufanya kuwa wafalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina***" ***(Ufunuo 1:5b-6).***

Damu inatumika namna gani kama silaha ambayo watakatifu wanaweza kutumia kumshida shetani na mshtaki?

Funguo za kufahamu haya ni ***dhambi zetu zimesamehewa*****!** Yesu alikufa kwa ajili yetu. "***Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote***" ***(1 Yohana 1:9).*** Mara tu dhambi zetu zinasamehewa na tumetakaswa na damu ya Kristo hakuna madoandoa au hukumu ya dhambi inabaki. ***Isaya 1:18 "Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji".*** **Kwa hivyo shetani hana msingi wa kushitaki.** "***lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu" 1 Wakorintho 6:11.*** Yawezekana tumehusika katika dhambi mbaya hapo awali lakini Mungu ametukomboa; ametuokoa na kutukomboa. Tuna ushindi juu ya dhambi; kwa hivyo tuna ushindi juu ya mauti ambayo ni msamaha wa dhambi; na tuna ushindi juu ya shetani na mapepo hayana msingi wa kutushtaki au kutugandamiza tunapotakaswa na kufunikwa na damu ya Mwana kondoo. **Tumia msaada ambao Mungu ametupa;** tambua nguvu za damu ya Yesu za kusamehe, kuosha na kulinda. Katika ***Kutoka 12*** damu juu ya mimo ya mlango ililinda manyumba kutoka kwa malaika wa kifo.

NENO LA USHUDA WAO (WETU)

Ushuda hutoka kwenye neno la Kiyunani shahidi. Mzizi wake ni *matur,* ambapo tunatoa neno la kingereza *martyr,* ambayo inamaanisha ***Yule aliye na ushuhuda kwa njia ya kifo.*** Ushuhuda ni zaidi ya kuongea ukweli wa injili; ni kuwa na ushahidi wa nguvu za kweli. Wazo hili ni sawa na

maelezo "***Maana ufalme wa Mungu hauwi katika neno, bali katika nguvu" 1 Wakorintho 4:20.*** Ushuhuda lazima uambatane na ujuzi wa mnenaji. Yohana anasema tunatangaza lile tulilo lisikia na tulililoliona na tulilolipapasa ***1 Yohana 1:1-3;*** kwa njia ingine tunacho shiriki ni kweli na hakika yake italeta mabadiliko kwa wasikizaji.

Hadithi ya kubadirishwa kwa Paulo imeandikwa katika **Mdo 9.** Katika **Mdo 22** Paulo anashuhudia juu ya hatua ya jeshi, ukishiriki ujuzi wa yale aliyoyapitia na vile alivyo kuja kumjua Yesu kama Masihi na Bwana. Tena katika ***Mdo 26,*** Paulo anashuhudia wazi mbele ya Agripa, akishiriki hadithi ya kugeuzwa kwake na kutumwa. Kwingineko katika maandiko Paulo anashuhudia, sio sana hadithi yake lakini akijumuisha jinsi Mungu amefanya kazi kupitia yeye na wengine. Mara kwa mara alihubiri na kufundisha neno katika njia ya ushuhuda: jinsi nguvu za Mungu zinafanya kazi, kulinganisha ufahamu wa maandiko kupitia yale yaliyo kuwa yakitendeka.
Yesu alisema juu ya ushuhuda wake akishuhudiwa na Baba (**Yohana 5:31-40).** Yesu aliahidi kuubeba ushahidi kwa ushuhuda wake ndani yetu kwa kudhibitisha ishara na maajabu (***Yohana 14:12-14 na Mariko 16:17-20).*** Neno la ushuhuda wetu ni kushiriki neno katika maisha yetu kutoka kwa ujuzi kamili. Ushuhuda hauwezi kukatalika. Ninaposhiriki ujuzi kamili unao eleza Neno na Roho akifanya kazi katika maisha yangu, hii ina nguvu sana. Hakuna nafasi ya shetani na mashtaka yake katika haya. Ni najua nimekutana naYesu! Ninajua Roho Mtakatifu ananiwezesha! Ninajua niko na Mamlaka juu ya shetani! Silitumii jina laYesu ambaye Paulo anamjua, ninatumia jina la Yesu ninaye mjua ***(Mdo 19:13-16).***

Juzi nilishiriki na kijana mdogo aliye vutwa kanisani. Yeye alikuwa wazi na mwenye moyo mwololo mbele za Mungu, lakini alikuwa hana ushuhuda. Hakumjua Bwana lakini alikuwa akitafuta. Akaniuliza, "watu wanajuaje nguvu za Mungu ndani yao? Ninaweza kumjua Mungu? Hiyo itanifanya kuwa tofauti na watu wengine?" na maswali mengine kama hayo. Huyo kijana aliomba nami, akimkiri Bwana na kuuliza nguvu za Roho Mtakatifu. Ninaamini atakuwa na neno la ushuhuda hivi karibuni.

- Je neno lako la ushuhuda ni lipi?
- Jambo la kutafakali: ungemjibu namna gani kijana huyu?

HAWAKUYAPENDA MAISHA YAO MPAKA KUFA

Nguvu kuu za shetani juu ya wanadamu tangia anguko ni hofu ya kifo. Yesu alisema usiogope wauao mwili wasiweze kuiua na roho; afadhali muogope Yule awezaye kuangamiza mwili na roho katika jehanamu ***(Mathayo 10:28).*** Kwa kifo chake Yesu aliangamiza Yule aliyekuwa na nguvu za kifo – huyo ni shetani – na kuwaweka huru wote wale waliokuwa wameshikwa katika utumwa kwa hofu yao ya kifo ***(Waebrania 2:14-15).***

Tunapomjia Yesu na kupatiana maisha yetu kwake kupitia rehema zake na neema, tunakufa kwa utu wetu wa dhambi na kufanyika hai kwa Mungu katika haki. Yesu anatukomboa kwa gharama kuu ya damu yake iliyo mwagika. Sisi sio mali yetu bali ya Mungu. Ni kupitia imani, kwaa neema tunaokolewa ***Waefeso 2:8.*** Tunapoelewa Yesu ni nani hakika na mambo yake yasio na ubishi kwa maisha yetu, na kuwa wanafunzi wake waliojitoa kwa moyo wote, tunakuwa tisho kwa shetani. Hile hali yetu ya kujipatiana kwa Mungu inamshinda yule mwovu (***Yakobo 4:7).*** Sasa ***maisha yetu yamefichwa ndani ya Kristo.*** Sisi ni milki yake. Tumehamishwa kutoka gizani

na kuingizwa katika utukufu wa nuru ya Mungu. Sasa sisi ni wana wa nuru. Giza haiwezi kufahamu au kushinda nuru.

Katika ***Mdo 1:8,*** Yesu alisema tutapokea nguvu mpya Roho Mtakatifu akija juu Yetu na tutakuwa mashahidi wake. Tutapata nguvu za Mungu ndani yetu za kushuhudia! Mungu atakua dhahiri ndani yetu. Kuwa shahidi itawezekana tu kupitia nguvu za Mungu ndani ya maisha yetu: hilo ndilo neno la ushuhuda wetu.

SILAHA ZINGINE

IMANI

1 Yohana 5:4-5: "kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu; na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?"
Yesu alifundisha juu ya nguvu ya imani ya kushinda:
Mariko 11:22-24 "Mwamini Mungu. Amin, nawaambia, ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. Kwa sababu hiyo nawaambia, yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu".

OMBI LA KUKUBALIANA

Hii inafuata kutoka kwa imani kwa kuwa imani iliyoshirikishwa ina nguvu kuliko imani ya mtu binafsi: ***Mathayo18:19-20: "Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao".***

KUFUNGA NA KUFUNGUA

Maombi ya kukubaliana yako katika mazingira ya kufunga na kufungua:
Mathayo 18:18: "amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni". Katika ***Mathayo 16:16-20*** kufunga na kufungua inapatianwa kama ufunguo katika ufalme wa Mbinguni na mazingila ni yale ya vita vya kiroho: ***"Wala milango ya kuzimu haitalishinda"*** kanisa ambalo limejengwa katika ufunuo wa imani ya Yesu Kristo.

JINA LA BWANA

Katika jina laYesu tunao ushindi! Bwana alisema tuombe kwa Jina lake. Bwana alisema atakuwa kati yetu tukiomba kwa makubaliano. Ni ombi la imani (kuamini katika jina lake) ambapo tunaomba. Mungu amempa Yesu "***jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina laYesu kila goti lipigwe la vitu vya mbinguni na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba" Wafilipi 2:9-11 pia waefeso 1: 19b -23.***

HITIMISHO

Kwa kujua na kutumia silaha ambazo Mungu ametupatia:

- Tunamshinda shetani (***ufu 12:11)*** na kusimama kinyume cha mbinu za shetani (***Efe 6:11);***

- Tunang'ang'ana kikamilifu na utawala na mamlaka na nguvu za mwovu katika ulimwengu wa roho ***(Efe 6:12):***

- Tunaangusha ngome na mawazo na kila kitu kilicho inuka juu ya maarifa ya Mungu ***(2 Wakorintho 6:4-5);***

- Tunaweza kuja kwa utiifu wa imani na kuwaelekeza mataifa katika kutii ***(2 Wakorintho 10:5b*** na ***Warumi 15:18)***

MAOMBEZI

MAOMBEZI – KITENDO CHA KWENDA KATIKATI.

Neno ombezi yamaanisha ***"Kitendo cha kwenda katikati".*** Yule afanyaye maombezi ni kama mpatanishi. Katika kuumba Mungu alimuweka mtu – Adam –hapa ulimwenguni kumuwakilisha yeye. Adamu alipewa wajibu kutawala "***ulimwengu wote***" (***Mwanzo 1:26, 28)***. Yeye alikuwa kama Yule aendaye katikati ya Mungu na viumbe vyake. Mtu alifanya dhambi na ikawa ni ya muhimu mtu apatanishwe na Mungu.

Kote katika agano la kale, maandiko yanakiri watu wa kiungu, wenye haki wakifanya maombezi ama wakipatanisha mtu mwenya dhambi au mwenye mahitaji na Mungu.
Abram aliomba kwa ukombozi wa watu wenye haki wa Sodoma (Mwanzo 18:23-36). Alifuatilia kuomba kwa sababu alijua tabia za Mungu – akapata jawabu kwamba Mungu alimkomboa Lutu na jamii yake kutoka uharibifu.
Musa alimuomba Mungu kwa msamaha wa wana wa Israeli *"**kwa hivyo Bwana akaughairi ule uovu aliosema ya kwamba atawatenda watu wake" (Kutoka 32:14) "na akafanya agano nao" Kutoka 32:9-15.***
Ezekieli 22:30: "nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu, lakini sikuona mtu". Mungu alikuwa akiangalia mtu atakayesimama katikati yake na mtu – atakaye uleta huo upatanisho kati ya Mungu na Mtu.
Isaya 59:16: "… Basi, mkono wake mwenyewe ndio uliomletea wokovu". Yesu akafanyika huyo mpatanishi.

YESU KAMA MUOMBEZI

Katika maisha yake hapa duniani, Yesu alidhihirisha (aliwakilisha) Mungu kwa mtu. Kisha kupitia kifo chake na kufufuka alikamilisha kazi yake kama vile alijitambulisha na mtu. Yeye aliwakilisha mtu kwa Mungu. Kazi iliyokamilika ya Yesu msalabani ilikuwa ya kutupatanisha na Mungu.

Yesu yuko wapi sasa na anafanya nini?

Katika **warumi 8:34,** Paulo anaandika, "***Kristo Yesu ndiye aliyekufa, naam, na zaidi ya hayo amefufuka katika wafu, naye ako mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea".*** Kwa kuwa aliishi kama mtu, alisimama pahali petu na akajitambulisha nasi na kwa hivyo yuko tayari sasa kutuwakilisha kwa Mungu. Anasimama mbele ya Mungu kutuwakilisha kwa Mungu kama mmoja wake – mwenye haki mbele ya uso wa Mungu. Huu ni wajibu wake kama ***mpatanishi.***

Waebrania 7:24-25: "…kwa kuwa akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiaye Mungu kwa yeye, maana yu hai sikuzote ili awaombee". Waebrania 9:24 yasema yeye yuko pale "***aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu".***

Kukubalika kwetu kunategemea hayo maombezi ya Yesu na kwa sababu yeye sasa anasimama mbele ya Baba kama kuhani tunaweza kuja kwa Mungu katika maombi "***tukiomba kwa jina lake".*** Kwa kuwa aonekana mbele ya Mungu kama kuhani, tunaweza kumfikia Mungu

kupitia yeye. Tunakuja kwa ujasiri kwa Baba kupitia Yesu Mwana wake na Kuhani wetu mkuu.
Yeye anapatanisha kati ya Mungu na mtu.
1 Timotheo 2:5: "kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu".

Katika kitabu chake "maobezi" Dutch sheets anapeana maelezo yafuatayo: "*maombezi ni sehemu ya huduma ya Yesu kupitia mwili wake, kanisa, ambapo tunapatanisha Mungu na mwanadamu kwa kusudi la kupatanisha ulimwengu kwake, au kati ya shetani na mwanadamu kwa kusudi la kuhamashisha ushindi wa Kalvari"*

Katika maombezi, kuna nafasi ya kuziita Baraka za Mungu katika maisha ya mtu mwengine. Tuna nafasi yakuulizaMungu ajithihirishe kwa hali fulani tunapo jua kwamba tunacho kiomba kinakubaliana na mapenzi yake. Tumeitwa kupatanisha: kusihi kwa rehema na haki kwa wengine; kuomba kwa ukombozi na uhuru wa wengine; kukataana na shetani kuingilia maisha ya wengine.
Tunapo hisi mzigo wa mtu mwingine twashiriki mateso ya huyo mtu. Tunakumbuka kazi ya Yesu iliyokamilika msalabani na ushindi alio mshinda shetani na kufufuka kwake kwenye ushindi tunapo mtafuta atuelekeze katika maombi. Tunakuja kwa maombezi kwa Yule tunayemjua, Yule, "***yuko mkono wa kuume wa Mungu, tena ndiye anayetuombea" Warumi 8:34.***

Yesu ametutuma ulimwenguni kama vile Baba alivyomtuma ulimwenguni (**Yohana 17:18, na 20:21).** Kwa hivyo nasi pia tumeitwa katika huduma hii ya maombezi – ***"kujenga ukuta na kusismama kwenye pengo***" kwa niamba ya wengine, kuwaakilisha wengine kwa Baba na kuonyesha ushindi ambao Yesu alishinda Kalvari.
Tunapomtazama tunapokea ahadi zake: **"*Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa" Yohana 15:7.***

KUKAA NDANI YA KRISTO YESU – KUOMBA KATIKA KUKUBALIANA
Twapaswa kujua maneno ya Yesu ili tujue mapenzi ya Baba, na kuomba kwa kukubaliana na mapenzi yake. Katika ***Yohana 14:10b*** Yesu alisema***, "Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake";*** na katika ***Ýohana 8:28 anasema, "Sifanyi neno kwa nafsi yangu, ila kama Baba alivyonifundisha ndivyo ninenavyo".***

Twahitaji kuwa pahali ambapo twasikia na kuona ambacho Mungu anataka kutenda katika maisha ya mtu ambaye tumekuwa tukiombea na katika hali ambayo tunaombea. Twaitanishwa na Yesu na mapenzi yake. Haya ndiyo Yesu alitenda alipokaa miongoni mwetu. Ijapo alikuwa Mungu (hivyo akaitanishwa na Mungu), pia aliitanishwa na Mtu. Tunapo uchukuwa mzigo wa mtu, tunatambulishwa au kushiriki katika mateso ya mtu huyo. (Tunaitanishwa na mtu).
Kisha tunatambulishwa na Yesu kupitia kazi yake iliyo kamilika aliyetenda Kalivari, twaweza kufanya maombezi kulingana na mapenzi na kusudi lake. Tunaomba kwa kukubaliana na mapenzi yake ***(Mathayo 18:19)***

Tunapomwendea Mungu kupitia Yesu kwa njia hii, tunapokea ahadi ambayo Yesu ametupa katika ***Yohana 16:23*** "***Mkimwambia Baba neno lolote atawapa kwa jina Langu"***
Twatakiwa kudumu (kukaa, kuishi, kuendelea) ndani ya Kristo Yesu na kumuuliza Mungu aachilie vipawa vya neno la unabii, hekima, maarifa na kupambanua, na kutupa maono na picha

– KUPOKEA KARAMA ZA ROHO KUTOKA KWA MUNGU ILI TUYAJUE MAPENZI YAKE.

Yesu kama muombezi katika maisha yake ulimwenguni

Waebrani 5:7 yatuambia: "Yeye, ***Siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi aliyokuwa mcha Mungu".*** Alituwekea mfano kwa Mda mwingi aliotumia katika maombi – wakati aliokaa katika uhusiano (alidumu) na Mungu na ambapo alijifunza mapenzi ya Baba yake.

Yesu atuoyesha jinsi tunapaswa kuomba tukimtazama akifanya maombezi kwa:

- **Waamini wadhaifu: "*Lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; naye utakapo ongoka waimalishe ndugu zako" Luka 22:32.***
- **Adui wake: "*Baba wasamehe kwa maana hawajui walitendalo" aya 34* .**
- **Kutumwa kwa Roho Mtakatifu: "*nami nitamuomba Baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele" Yohana 14:16.***
- **Kwa ajili ya kanisa:** (Wanafunzi wake wakati huu na wakati ujao): ***Yohana 17:***
  Aya 9: "*Mimi nawaombea hao; siuombei ulimwengu; bali hao ulionipa kwa kuwa hao ni wako".*
  Aya 11: "… kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo".
  Aya 15: "Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu".
  Aya 17: "uwatakase kwa hile kweli".

Yesu asema nini katika ***Mathayo 9:37-38?***
Anatupa maagizo ***Tuombe ili Mungu alete wakristo watenda kazi.*** Katika kuyatenda haya amelituma kanisa kupatanisha katika maombi.

Katika kuugua kwake tunamuona akiomba kwa ajili ya wokovu wa wengine. "***Naye kwa vile alivyokuwa katika dhiki, akazidi sana kuomba; hari yake ikawa kama matone ya damu yakidondoka nchi" Luka 22:42-44.*** Kuugua huku kumenakiliwa katika ***Mariko 14:34,*** na katika ***Mathayo 26:38***. Katika vifungo hizo viwili Yesu anawauliza wanafunzi wake "***kaeni hapa, mkeshe pamoja nami".*** Pia kuna mfano wetu wa kuzingatia – Yesu, kwa maombezi, alitafuta msaada wa wengine.

Katika kumfufua Lazaro kwa wafu (**Yohana 11:1-44),** Yesu alifanya maombezi kwa kuugua na machozi:

Aya 33: "***Aliugua rohoni, akafadhaika roho yake"***
Aya 35: "Yesu akalia machozi"
Aya 38: "Basi Yesu, hali akiugua tena nafsini mwake…"
Aya 41: "Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia" Baba alisikia nini?
Aya 43: "Akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje!".

Yesu alifundisha juu ya maombi.

Kupitia mfano wa mjane aliyekuja kwa hakimu mwenye moyo mgumu ***(Luka 18:1-8),*** na mfano wa rafiki aliyetembea usiku wa manane ***(Luka 11:1-10***), Yesu alitufundisha kufuatilia katika maombi. "***Kisha Yesu akawaambia wanafunzi wake mfano kuwaonyesha waombe bila kukoma" Luka 18:1.***

Pia alitufundisha ***kutarajia Mungu ajibu*** maombi Yetu aliposema, "***Lolote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni" Yohane 15:16.*** Hii ina masharti kulingana na kudumu kwetu ndani ya Kristo.

Mtume Paulo, aliandika kwa Timotheo akihimiza umuhimu wa kutarajia na kufuatilia katika maombi. Katika ***1 Timotheo 2:1*** Paulo anasema, "***Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote".***

Kutarajia kitu kutoka kwa Mungu yahitaji kumtumaini Mungu na uaminifu wake kuweka ahadi zake. Hata kabla ya hajajibu tunaweza kumpa shukrani kwa taraja. Katika ***Wafilipi 4:6,*** Paulo anawahimiza waamini "… ***katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu"***

Omba, tarajia, na utazamie jawabu.

Haya matarajio yanakuja kwa kujua asiri ya Mungu Yule tunayemuomba. Twajua ya kwamba yeye ni Mungu anayeweka ahadi zake na ni wa rehema na huruma Mungu apendaye haki. Tazama maombi haya ya mtume Paulo katika ***Waefeso 6:18-20.***

Aya 18 "Kwa watakatifu.
Aya 19-20 Kwake yeye kama ***Mhubiri mmishonari.***

Tazama kwa maombezi ***kwa watakatifu*** katika ***Wafilipi 1:9-10, Waefeso 3:16:19*** na maombezi kwa watu wote katika ***1 Timotheo 2:1-4.***

Tuna uhakika ya kwamba tunaweza kuomba maombi haya kwa maana yanaeleza mapenzi ya Mungu kama vile anasema katika maandiko. Kama kanisa mwili wa Yesu, yatupasa kufuatilia katika maombi haya na tushukuru katika kutarajia Mungu kutimiza ahadi yake.

<u>Maombezi ndani ya Roho.</u>

Katika **Yohana 17:21,** Yesu alituombea ili tuwe na umoja na Baba kama vile yeye na Baba walivyo mmoja. Tunapojitoa kwa Mungu na utu wetu kufa, Roho Mtakatifu anaweza kutembea huru ndani ya maisha yetu. Tunampa haki kujidhihirisha katika miili yetu – kujieleza kama achaguavyo.

Paulo anaandika katika ***Warumi 8:26-27: "kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo; lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusiko weza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu."*** Paulo anasema ya kuwa Roho anaomba kupitia roho zetu bila kuingilia utu wetu. Maombi haya ndani ya Roho ni ni mapenzi ya Mungu safi, kwa sababu ni maombezi ya Roho, sio yetu. Baraka gani hii ! Mungu anafunika upungufu wetu katika maombi.

DHIHIRISHO

Paulo anaandika kwamba "***Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana"*** (***1 Wakorintho 12:7).***

Dhihirisho ni ishara ya vipawa ambazo Roho Mtakatifu anapatiana, na vipawa hivi vimeandikwa katika ***1 Wakorintho 12:8-9.*** Vipawa tutakavyoangalia katika fundisho hili ni kazi inayofanyika ya mzigo ambao Mungu anatupa. Hazina kitu cha kufanya na msisimuko wa kawaida, na mara kwa mara zinakuja bila onyo/ilani. Ni ishara za Roho akifanya maombezi kwa ajili yetu. Miili yetu Inajilainisha na Roho jinsi tunavyo simama inaathiliwa. Dhihirisho inawezekana kuwa kelele kama (kuugua na kulia)

UCHUNGU:

Mojawapo ya dhihirisho ambayo tunaona yaweza kulinganishwa na matayarisho ya mwanamke wakati wake unapofika kabla ya kijufungua:

- **Utungu unaanza bila ilani;**
- **Mama analia kwa utaratibu;**
- **Mtoto haji kabla ya wakati wake – hauwezi kuharakisha hatua;**
- **Wengine wako kumsaidia mama kujifungua;**
- **Kuna furaha mtoto anapozaliwa.**

Maandiko yaonyesha ***uchungu huu*** na unashughulikia kuzalisha kitu katika ulimwengu wa rohoni.

Tunamwona Yesu akilia, jasho yake ikidondoka kama matone ya damu, akiugua ndani ya Roho kama vile aliugua katika bustani ya Gethisemane. Aliuliza wanafunzi wake wakae naye na kumfariji kwa yale aliyoyapitia. Alinena kuhusu furaha iliyokuwa mbele yake (ijapokuwa wanafunzi hawakuelewa na kuhisi hiyo furaha kwa mda).

Bwana hutazama maombezi haya ya kuzalisha kitu katika ***Yeremiah 4:31:*** "***kwa maana nimesikia sauti, kama sauti ya mwanamke wakati wa utungu wake, na sauti yake aumwaye, kama mwanamke azaaye mtoto wake wa kwanza, sauti ya binti Sayuni, atwetaye kupata pumzi, na kunyosha mikono yake"***

Isaya 26:17 yasema "***Kama vile mwanamke mwenye mimba anayekariba wakati wake wa kuzaa, alivyo na utungu na kulia kwa sababu ya maumivu yake, ndivyo tulivyokuwa mbele zako Ee BWANA.***

Katika ***1 Wafalme 18:42*** tunamuona Eliya juu ya mlima Karimeli akichukua nafasi kama mwanamke aliyekaribia kuzaa anapomngojea Mungu kutimiza ahadi zake.

Mtume Paulo anazungumzia juu ya ***"Vitoto vyangu, ambayo kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani Yenu" Wagalatia 4:19.***

Kujidhihirisha huku kwa uchungu huja wakati tunatambua katika hali ionekanayo na njia ambayo Mungu ameweka katika maeneo ya mbinguni kuzalisha kitu.

NDIMI

Kipawa hiki mara kwa mara huachiliwa kusaidia maombezi. Roho wa Mungu anaelewa tunachohitaji kuombea na jinsi itupasavyo kuomba. Kuomba kwa ndimi wakati dhihirisho lingine li juu ya mtu mara kwa mara yatupa kuelewa ni nini kinachotendeka.

MACHOZI
Yesu alilia katika bustani ya Gethisemane ***(Luka 22:44),*** na pia katika kaburi ya Lazaro (***Yohana 11:35).***
Paulo aliwalilia wengine. Katika ***2 Wakorintho 2:4*** anasema, "***maana katika dhiki nyingi na taabu ya moyo niliwaandikia na machozi mengi …"*** na katika ***Wafilipi 3:18***, ***anaandika: "maana wengi hueneda, ambao nimewaambieni mara nyingi habari zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi…"***
Bwana ameahidi kwamba "***Watavuna kwa kelele za furaha. Ingawa mtu anakwenda zake akilia azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha aichukuapo miganda yake" Zaburi 126:5-6.***

Dhihirisho nyingine zilizotajwa katika maadiko

Musa ***alianguka chini*** mbele za Bwana akimsihi kwa sababu ya watu baada yao kutenda dhambi ***Kum 9:18***. Nguvu za asili za Danieli zilimuishia na: "***ndipo nikashikwa na usingizi mzito, na uso wangu ameielekea nchi" Danieli 10:9.***
"***Ibrahimu alikuwa akali akisimama mbele za Bwana" Mwanzo 18:22*** alipokuwa akimsihi Mungu kwa sababu ya sodoma. Kuna wazo la **kungojea** wakati mfalme Sulemani "***aliposimama mbele ya madhabahu ya Bwana" 2 Nya 6:12*** kumsihi Mungu atimize ahadi alizompa mfalme Daudi.
Nehemaya "***Aliomboleza na kufunga na kuomba mbele za Mungu wa mbinguni" Nehemia 1:4*** kama alivyo waombea watu na pendekezo lake alilotoa kwa mfalme.

TAMATI.
Katika 'Rees Howells: muombezi', Norman Grubb aliandika '*wakati Roho Mtakatifu anaishi maisha yake ndani ya chombo kiteule, hakuna kipimo cha kule atampeleka, katika juhudi zake za kuonya na kuokoa waliopotea'*. Anazungumza juu ya:

- **Isaya aliitwa aende "uchi na bila viatu"** kama onyo kwa wa Israeli;
- **Hosea** alimuoa kahaba kama ishara ya kuonyesha vile Mungu alitamani kuwachukua watu wake waliofanya usherati.
- **Yeremia** ambaye hakuruhusiwa kuoa kama onyo kwa waisraeli dhidi ya hofu na maovu ya kuwa mateka.

Haya na mifano mingi katika maandiko yatuonyesha vile roho mtakatifu atatumia mtu aliyejitolea kuyaombea mataifa yote. Watu wengi katika agano la kale wamefanya maombezi kwa rehema na Baraka, kuachiliwa kutoka kwa aibu, na msamaha wa dhambi na matokeo makubwa.
Katika historia tumemuona **wesley** akiombea wingereza iliyoanguka, **William Booth** kwa panda na shuka, **Hudson Taylor** na ndugu **Andew** kutoka China, **Ed Silvosa** wa Argentina…kuwataja wachache tu.

Kwa mda mrefu, kipawa cha uombezi hakikuonekana katika mikutano ya hadhara.
Waliofanya maombezi kwa msukumo na kufuatilia kwa jumla waliomba kibinafsi. Roho Mtakatifu amebadilisha mambo mengi katika maisha ya kanisa karibuni na Mungu Roho Mtakatifu anaachilia watu zaidi na zaidi katika uhuru ili wafanye kazi hii nzuri ya maombi. Katika makanisa mengi na miji kuna vikundi spesheli za maombezi ambapo watu na pia watoto

wanamgojea Bwana kuona vile Bwana anataka waombe na kuachilia mapenzi yake katika maisha yao binafsi na taifa.

Mungu amemaanisha katika kusudi lake la kuleta ufufuo na kuyaleta mavuno. Malengo haya yanapokua hakika katika mioyo yetu, kuitikia kwetu ni kulia na kuugua, uchungu mpaka alete kile anatamani. Mungu anaweka ndani ya mioyo yetu msukumo wa walio potea, na anatuita kwa upendo wake wa kwanza.

ZOEZI

Kusudi la zoezi hili ni kujipatiana kwa Roho wa Mungu na kumruhusu alete mzigo wa maombezi juu yetu; kisha kufuata mzigo huu katika kikundi (mkisaidiana) kuomba mpaka uwe na amani apatianayo Mungu kama ishara ameyasikia maombi yetu.

Muulize Roho Mtakatifu -
- ***Ayazamishe maombi yetu.***
- ***Aachilie mzigo wa watu waliopotea.***
- Kuachilia ***msukumo*** wa ***usafi*** na ***utakatifu*** ndani yetu na mwili wa kristo wote.
- Aachilie msukumo wa ufufuo uje.

Omba kwa Roho wa "***neema na kuomba" (Zekariah 12:10).*** Kiongozi anaweza kuhudumu kupitia kuwekea watu mikono kuachilia kipawa.

Njia moja ambayo Roho mtakatifu anajibu kwa maombi haya, ni kuweka mzigo wa maombi kwa mtu kupitia kudhihirika ambako hajapitia tena. Haya yanapofunguka, tunawahimiza wengine kukusanyika kwa yule aliye na mzigo na kumsaidia mtu huyo katika maombi kwa kipawa chochote atakacho achilia Roho mtakatifu kwa kila mtu.